



Kwa Wadau wa Sekta ya Ununuzi wa Umma.

**SHUKRANI KWA KUSHIRIKI NA KUFANIKISHA
WIKI YA UNUNUZI WA UMMA**

1. Kama unavyokumbuka, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma nchini, iliandaa Wiki ya Ununuzi wa Umma kuanzia tarehe 05 – 07 Mei, 2022 Jijini Arusha. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma (PPAA), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB). Tukio hilo lilizinduliwa Rasmi mnamo Tarehe 5 Mei, 2022 na **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**.
2. Katika tukio hilo lililokuwa na Kaulimbiu “**Matumizi ya Teknolojia katika Kuboresha Ununuzi wa Umma**” kulifanyika Kongamano la Wadau wa Ununuzi wa Umma lililofanyika kuanzia tarehe 05 – 07 Mei, 2022 na kuhudhuriwa na wadau wapatao 1,140. Pia, kulifanyika zoezi la Kurejesha kwa Jamii (CSR) ambapo Taasisi wenyeji zilitoa mafunzo ya fursa zinazotolewa na Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa Makundi Maalum (Wanawake, Vijana, Wazee na Watu Wenye Ulemavu).
3. Kwa niaba ya Kamati ya Maandalizi ya Wiki ya Ununuzi wa Umma, ninayo heshima kubwa kuwashukuru kwa kufanikisha Kongamano hilo. Mada zilizowasilishwa pamoja na Maazimio ya Washiriki yanapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka www.ppra.go.tz na www.taneps.go.tz.
4. Tunawashukuru na tunaamini ushirikiano huo utaendelea. Mungu awabariki sana.

Wenu katika Ujenzi wa Taifa;

Dkt. Irene C. Isaka

AFISA MTENDAJI MKUU PPRA NA
MWENYEKITI WA KAMATI YA MAANDALIZI
10 Mei, 2022